JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2023

# STADI ZA KAZI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU

## DARAJA LA A (GATCE) 2023

# 634 STADI ZA KAZI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI. .... 2

2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi. ........ 2
2.1.1 Swali la 1: Ufundishaji wa Mada Teule. ........ 2
2.1.2 Swali la 2: Ufundi ........ 4
2.1.3 Swali la 3: Udobi ........ 7
2.1.4 Swali la 4: Muziki ........ 9
2.1.5 Swali la 5: Sanaa za Maonesho ........ 11
2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Ufundishaji. ........ 13
2.1.7 Swali la 7: Maandalizi ya Ufundishaji ........ 16
2.1.8 Swali la 8: Upishi ........ 18
2.1.9 Swali la 9: Kilimo, Ufugaji na Uvuvi ........ 21
2.1.10 Swali la 10: Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo ........ 23
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha ........ 25
2.2.1 Swali la 11: Ushoni wa Nguo ........ 25
2.2.2 Swali la 12: Upimaji ........ 29
2.2.3 Swali la 13: Ufundishaji wa Mada Teule. ........ 34
2.2.4 Swali la 14: Biashara Ndogo ndogo. ........ 40

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA ... 44

4.0 HITIMISHO ........ 44

5.0 MAPENDEKEZO ........ 45

Kiambatisho ........ 46

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Mtihani wa kuhitimu Mafunzo ya Ualimu Daraja la A kwa somo la Stadi za Kazi kwa mwaka 2023. Taarifa hii inakusudia kutoa mrejesho wa ufaulu wa watahiniwa kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera, wakuza mitaala na wadau mbalimbali wa elimu. Mtihani ni zana mojawapo inayotumika kutathmini na kutoa hitimisho katika mchakato wote wa ufundishaji na ujifunzaji hivyo, majibu ya watahiniwa katika mitihani huonesha viwango vya uwezo wa kufikiri, ubora wa mielekeo, stadi na maarifa ambayo watahiniwa waliweza kuyapata katika miaka miwili ya mafunzo ya Ualimu.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kutoa uelewa wa sababu zilizofanya watahiniwa kujibu maswali vizuri au kushindwa kujibu vizuri. Watahiniwa walio wengi walifanya vizuri katika mtihani wa somo la Stadi za Kazi. Watahiniwa hao walikuwa na ujuzi wa kutosha katika mada mbalimbali zilizotahiniwa, uwezo mzuri wa kubaini matakwa ya swali pamoja na uwezo wa kujibu maswali kulingana na nyanja husika. Vilevile watahiniwa walikuwa na maarifa ya kujenga hoja sahihi katika kujibu maswali yaliyoulizwa.

Hata hivyo, sababu za kushindwa kujibu vizuri katika baadhi ya maswali zimeainishwa ikiwemo kutobaini matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha katika baadhi ya mada, kutoa ufafanuzi usiojitosheleza na kutozingatia maelezo yaliyotolewa kwenye swali. Aidha, watahiniwa hao walikosa umahiri wa kujieleza katika mtiririko unaoleta mantiki na kushindwa kuandika sehemu za utangulizi na hitimisho hususan katika maswali ya insha.

Ni matarajio ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, wakuu wa vyuo, wathibiti ubora wa shule, wakufunzi na wanachuo kupata mbinu muafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani na wote walioshiriki katika maandalizi ya taarifa hii.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Stadi za Kazi kwa watahiniwa wa mtihani wa Ualimu Daraja la A uliofanyika Mei 2023, uliandaliwa kwa kuzingatia Muhtasari wa somo la Stadi za Kazi wa mwaka 2009 na fomati ya mtihani wa mwaka 2023.

Mtihani huu ulikuwa na jumla ya maswali kumi na nne (14) yaliyogawanywa katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ya majibu mafupi kutoka katika mada za taaluma na ufundishaji ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na maswali manne (04) ya insha kutoka katika mada za taaluma na ufundishaji ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu A ilikuwa na jumla ya alama arobaini (40) ambapo kila swali lilikuwa na alama nne (04). Sehemu B ilikuwa na jumla ya alama sitini (60) ambapo kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15).

Ufaulu wa watahiniwa katika somo la Stadi za Kazi kwa mwaka 2023 ulikuwa mzuri kwani kati ya watahiniwa 4,354 (100%) waliofanya mtihani, watahiniwa 4,353 (99.98%) walifaulu kwa kupata alama 40 na zaidi. Kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani asilimia 11.7 walipata Daraja A, asilimia 63.4 walipata Daraja B, asilimia 24.5 walipata Daraja C, asilimia 0.4 walipata Daraja D na asilimia 0.02 walipata Daraja F. Kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2023 kimepungua kwa asilimia 0.02 ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 100.

Ufaulu wa watahiniwa katika taarifa hii umegawanywa katika viwango vitatu ambavyo ni ufaulu mzuri unaoanzia alama 70 hadi 100, ufaulu wa wastani alama 40 hadi 69 na ufaulu hafifu alama 0.0 hadi 39. Chati za viwango vya ufaulu na rangi zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu wa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano ufaulu wa wastani na rangi nyekundu ufaulu hafifu.

Taarifa hii inachambua kwa kina maswali yenye ufaulu mzuri, wastani na hafifu pamoja na sababu zilizowafanya watahiniwa kupata ufaulu huo. Sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa ili kuonesha majibu waliyofanya vibaya na waliyofanya vizuri. Hivyo, uchambuzi huu utasaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi kwa mada ambazo ufaulu ulikuwa wa wastani ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika mitihani yao.


## 2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu A ilikuwa na maswali ya majibu mafupi kumi (10) kutoka katika mada za: *Ufundishaji wa Mada Teule, Ufundi, Udobi, Muziki, Sanaa za maonesho, Misingi ya Ufundishaji, Maandalizi ya Ufundishaji, Upishi, Kilimo, ufugaji na uvuvi* na *Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo*. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na jumla ya alama nne (04) ambapo ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu (03); kundi la kwanza ni ufaulu wa kiwango kizuri wa kuanzia alama 3.0 hadi 4.0, ufaulu wa wastani alama 2.0 hadi 2.5 na ufaulu hafifu alama 0.0 hadi 1.5.

#### 2.1.1 Swali la 1: Ufundishaji wa Mada Teule


Swali liliwataka watahiniwa kueleza kwa ufupi mbinu nne za kutumia kufundisha mada ya ufugaji bora wa kuku wa kienyeji kwa wanafunzi wa Darasa la Saba. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 3,156 (72.49%) walipata 3.0 hadi 4.0, watahiniwa 792 (18.19%) alama 2.0 hadi 2.5 na watahiniwa 406 (9.32%) alama 0.0 hadi 1.5. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Ufaulu wa jumla wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 3,948 (90.68%) walifaulu kwa kupata kuanzia alama 2.0 hadi 4.0.


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa ufaulu mzuri wa watahiniwa ulisababishwa na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ufundishaji wa mada teule hususani ufundishaji wa ufugaji wa kuku wa kienyeji. Pia, watahiniwa hao walibaini matakwa ya swali. Baadhi ya mbinu sahihi walizoeleza kwa ufasaha zilikuwa: *Mbinu ya ziara, mbinu ya kujozisha, mbinu ya kualika mgeni, majadiliano* na *mbinu ya kisa mafunzo.* Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.


1 Mbinu za ufundishaji wa somo la ufugaji bora wa kuku wa kienyeje ni:-
i) Mbinu ya maswali na majibu mf. nitauliza nini maana ya ufugaji?
ii) Majadiliano ya vikundi, hii huhusisha kubadilishana mawazo kuhusu somo mf. kujadili maana ya ufugaji.
iii) Mbinu ya ziara, pia nitatumia ziara mfano kwenda kutembelea sehemu wanapofuga kuku wa kienyeji.
iv) Onesho mbinu, ambayo huhusisha kuonesha mfano wa kile kinachojifunzwa.

**Kielelezo Na. 1.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani waliweza kubaini matakwa ya swali ila walishindwa kueleza mbinu nne za kutumia kufundishia mada ya ufugaji bora wa kuku wa kienyeji kwa wanafunzi wa Darasa la Saba. Baadhi ya watahiniwa walieleza kwa ufupi mbinu mbili badala ya nne na wengine walichanganya kwa kueleza mbinu sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa mbinu nne kama vile: *Mbinu ya muhadhara, mbinu ya matembezi ya galari, mbinu ya ziara ya mafunzo* na *mbinu ya kualika mgeni*. Mtahiniwa huyu alishindwa kubaini kuwa *mbinu ya muhadhara* na *mbinu ya matembezi ya galari* haziwezi kutumika kufundishia mada ya ufugaji wa kuku wa kienyeji kwa wanafunzi wa Darasa la Saba kwa kuwa mbinu hizo hutumika katika ufundishaji wa mada za Misingi ya Ufundishaji na ufundishaji wa mada ya uimbaji.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu, baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mbinu za ufundishaji hivyo walieleza mbinu zisizo sahihi. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa alieleza: *Mbinu ya changanya kete, mbinu ya matembezi ya galari* na *mbinu ya bungua bongo.* Mtahiniwa hakuelewa kuwa mbinu hizo haziwezi kufanikisha ufundishaji wa mada hiyo kwa kuwa haziwezeshi wanafunzi kujenga umahiri wa ufugaji bora wa kuku wa kienyeji. Mtahiniwa mwingine alifafanua mbinu za upimaji ambazo hutumika katika kupima ufundishaji wa mada ndogo za Uchambuzi wa Muhtasari na Uchapaji kwa njia ya kimia kama vile: *Orodha hakiki* na *mbinu ya Fomu ya uchunguzi*. Kelelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.


1 i) Kuandaa banda (kwa kufanya ziara ya utengenezaji wa banda

ii) Kuandaa vifaa (kwa kufanya manunuzi ya vifaa mfano. vyombo vya maji, masinia

iii) Kuandaa chakula cha kuku mfano makombo pumba.


iv) Kuanda sehemu ya kutagia kuku mfano mayai.

**Kielelezo Na. 1.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 1.2 mtahiniwa alieleza hatua za kuzingatia wakati wa kuanzisha shughuli ya ufugaji wa kuku wa kienyeji badala ya mbinu za kutumia kufundishia mada ya ufugaji bora wa kuku wa kienyeji kwa wanafunzi wa Darasa la Saba.

### 2.1.2 Swali la 2: Ufundi


Swali liliwataka watahiniwa kufafanua vifaa vinne vya matengenezo ya baiskeli na kazi zake. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 3,199 (73.47%) walipata 3.0 hadi 4.0, watahiniwa 440 (10.11%) alama 2.0 hadi 2.5 na watahiniwa 715 (16.47%) alama 0.0 hadi 1.5. Chati Na 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 3,639 (83.58%) walifaulu kwa kupata kuanzia alama 2.0 hadi 4.0.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ufundi wa baiskeli hivyo kufafanua kwa usahihi vifaa vya matengenezo ya baiskeli na kazi zake. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua vifaa hivyo na kazi zake kama vile: *(a) Spana ambayo hutumika katika kazi ya kufunga na kufungulia nati mbalimbali, (b) Koleo ni kifaa ambacho hutumika kushikia na kung'olea vifaa mbalimbali, (c) Pampu hutumika katika kujazia upepo kwenye mpira wa ndani wa tairi la baiskeli* na *(d) Grisi husaidia kupunguza au kuondoa msuguano kwenye baiskeli.* Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.


2 Msasa laini. Hiki ni kifaa kimoja wapo ambacho hutumika kusugulia na kutoa uchafu kwenye tubu (mpira) ilikusaidia kukaa kwa gundi wakati wa kuziba pancha.

Spana. Hiki ni kifaa cha matengenezo katika baiskeli ambacho kinakaziya kufungua boliti na skruu

Grisi (mafuta yamashine.). Pia hiki ni kifaa ambacho kinakazi ya kupunguza msuguano katika maungio ya baiskeli au kulainisha nyororo pia kuiepuska isipatwe na kutu.


Pampu. Kujaza upepo (hewa) kwenye taili

Nyundo. Kugongelea au kupashindilia pale panapo achia.

**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2.

Vile vile, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani baadhi yao walichanganya vifaa sahihi na visivyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya vifaa vya matengenezo ya baiskeli na vifaa vinavyotumika katika matengenezo ya viatu kama vile: *(a) spana - hutumika kukaza sehemu ya baskeli iliyoharibika*, *(b) dawa - hutumika kugandishia kwenye kipande cha nyuzi katika sehemu iliyotoboka*, *(c) kisu - hutumika kukatia kipande cha nyuzi* na *(d) gurudumu la baiskeli - hutumika kubadilisha kama lile la awali limepasuka.* Maelezo ya vifaa kama vile: *dawa* na *kisu* ni kwa matengenezo ya viatu wakati vifaa kama: *spana* na *gurudumu* ni kwa matengenezo ya baiskeli. Aidha, watahiniwa wengine hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ufundi hivyo walieleza vifaa vichache vya matengenezo ya baiskeli na kazi zake. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walifafanua vifaa viwili pekee na wengine walitaja vifaa hivyo bila ufafanuzi wa kazi zake.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu wengi wao walishindwa kubainisha na kufafanua vifaa vinne vinavyotumika katika matengenezo ya baskeli. Watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali na wengine kukosa maarifa juu ya vifaa husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja vifaa vinavyotumika kuunda baskeli kama vile: *tegete*, *midenge*, *taili* na *sumaku* badala ya vifaa kama: *spana*, *koleo*, *pampu* na *grisi.* Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.



2

i) Sindano

ii/ uzi

iii/ Mavazi ya kazi

iv) Mbao ya kupima mguu wa mteja:

**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.2 mtahiniwa alitaja vifaa vinavyotumika katika matengenezo ya viatu badala ya vifaa vya matengenezo ya baiskeli na kazi zake.

### 2.1.3 Swali la 3: Udobi

Swali hili liliwataka watahiniwa kueleza manufaa manne watakayopata wanafunzi kutokana na kufua nguo zao mara kwa mara. Swali lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 4,124 (94.72%) walipata 3.0 hadi 4.0, watahiniwa 204 (4.69%) alama 2.0 hadi 2.5 na watahiniwa 26 (0.60%) alama 0.0 hadi 1.5. Jedwali Na. 1 linaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.


**Jedwali Na. 1: Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3**

| Na. | Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 1. | 0.0 – 1.5 | 26 | 0.60 |
| 2. | 2.0 – 2.5 | 204 | 4.69 |
| 3. | 3.0 – 4.0 | 4,124 | 94.72 |

Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 4,328 (99.41%) walifaulu kwa kupata kuanzia alama 2.0 hadi 4.0.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya udobi. Watahiniwa hao waliweza kubaini matakwa ya swali na hivyo


walifafanua manufaa watakayopata wanafunzi kutokana na kufua nguo zao mara kwa mara kama vile: *Kuondoa harufu mbaya katika nguo, kuzifanya nguo zidumu kwa muda mrefu, kuzifanya nguo kuwa safi na kumfanya mvaaji kuonekana nadhifu* na *kuua vijidudu vinavyosababisha magonjwa mfano fangasi na harara*. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.


3 Zifuatazo ni faida za kufua nguo.
(a) Kupendezesha: mtu anapofua nguo na kuondoa uchafu huifanya nguo hiyo kuwa na thamani ya hali ya juu na kupendeza.
(b) Kuondoa vijidudu vya magonjwa: Watu wanapofua nguo husaidia kuondoa vimi ambao wanaweza kusababisha vimi ya magonjwa.
(c) Kuondoa harufu mbaya: Nguo inapokuwa chafu huwa na harufu mbaya kutokana na jasho pamoja na uchafu hiyo tunapofua tunaondoa iyo harufu.
(d) Kuepusha nguo kuchakaa haraka: Hii ni kwa sababu nguo inapokaa na uchafu hupelekea kuchakaa - tofauti na ikiwa imefuliwa maana itaonekana mpya.

**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3.

Vile vile, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani baadhi yao walieleza manufaa mawili kati ya manne yaliyotakiwa. Wengine walichanganya manufaa ambayo mwanafunzi anaweza kuyapata kwa kufanya kazi ya udobi na manufaa ya kufua nguo mara kwa mara. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama vile: K*ujipatia kipato, kujipatia ajira, kuwa nadhifu* na k*uzifanya nguo zidumu.* Hoja ya *kujipatia kipato* na *kujipatia ajira* ni faida anayoweza kuipata mwanafunzi kwa kufanya kazi ya udobi lakini siyo manufaa ya kufua nguo mara kwa mara, hivyo alipata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walishindwa kubaini matakwa ya swali na wengine kutoa hoja zisizo sahihi. Baadhi ya watahiniwa walieleza kanuni ambazo dobi anapaswa kuzingatia wakati wa kufua nguo kama vile: K*ufahamu hatua za udobi, kufahamu aina na alama mbalimbali zilizopo kwenye nguo kwa mfano alama ya kufua kwa kutukia jiki*. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.



3

(i) Kusaidia nguo isi chakae mapema, kwa-
nguo "ikifufiwa mara kwa mara huweza
kuchakaa zaidi.
(ii) Kufua nguo kila mara kunapunguza-
ubora wa nguo.

(iii) kufua nguo kila mara hufanya nguo-
ichanike kwa urahisi.


(iv) Kufua nguo kunaongeza gharama. Kwani
matumizi ya sabuni, maji yatakuwa yana-
tumika zaidi

**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.2 mtahiniwa alieleza madhara ya kufua nguo mara kwa mara badala ya manufaa ambayo wanafunzi wanaweza kuyapata kutokana na kufua nguo zao mara kwa mara.

### 2.1.4 Swali la 4: Muziki


Swali liliwataka watahiniwa kufafanua kwa ufupi makundi manne ya ala za muziki. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 2,635 (60.52%) walipata 3.0 hadi 4.0, watahiniwa 320 (7.35%) alama 2.0 hadi 2.5 na watahiniwa 1,399 (32.13%) alama 0.0 hadi 1.5 kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Ufaulu wa jumla wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa watahiniwa 2,955 (67.87%) walifaulu kwa kupata kuanzia alama 2.0 hadi 4.0.


Watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muziki. Vile vile, watahiniwa hao walibaini matakwa ya swali hivyo, waliweza kufafanua kwa ufupi makundi ya ala za muziki kama: *(a) Ala za kugusa; ala hizi huchezwa kwa kutumia vidole vya mikono kwa njia ya kugusa au kuparuza ili kupata sauti itakayoongoza katika uimbaji. Mfano wa ala hizi ni gitaa (b) Ala za kugonga; ala hizi huchezwa kwa njia ya kugonga kwa kutumia vidundo vipande vya miti ili kupata sauti itakayoongoza uimbaji. Mfano wa ala hizi ni ngoma (c) Ala za kubonyeza; ala hizi huchezwa kwa kutumia vidole vya mikono kwa njia ya kubonyeza ili kupata sauti itakayoongoza uimbaji. Mfano wa ala hizi ni kinanda (d) Ala za kutikisa; ni ala ambazo zipo katika kundi la ala za kutikisa ambayo huchezwa kwa njia ya kutikisa kwa mikono/ mkono mmoja ili kupata mwendo wa muziki. Mfano wa ala hizi ni manyanga na kayamba* na *(e) Ala za kupuliza; ala hizi huchezwa kwa njia ya kupuliza kwa mdomo ili kupata sauti ambayo itaongoza muziki na kuleta mwafaka mzuri. Mfano wa ala hizi ni kama vile filimbi, zumari* na *baragumu*. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.


4 Makundi ya ala za muziki ni:-
i/ Ala za kugonga: Ni ala ambazo hutoa sauti zi napogongwa mf. ngoma
ii) Ala za kupuliza: Ni ala zinazotoa muziki kwa kupulizwa mf. filimbi
iii) Ala za kutikisa: Ni ala zinazotoa muziki kwa kutikiswa mf. junga.
iv) Ala za kukwaruza: Ni ala zinazotoa muziki kwa kukwaruza mf. marimba, gitaa

**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walionesha kuwa na maarifa ya wastani kuhusu muziki. Baadhi ya watahiniwa waliweza kufafanua makundi machache ya ala za muziki huku wengine wakichanganya na vifaa vingine vinavyotumika katika muziki ambavyo siyo makundi ya ala za muziki.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muziki hivyo kushindwa kufafanua makundi sahihi ya ala za muziki. Wengine walifafanua dhana ambazo hutumika katika muziki lakini hazikuulizwa katika swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *Sapran, atles, septo* na *bass* ambazo ni dhana zinazotumika katika muziki badala ya makundi manne ya ala za muziki. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.


4

i) Ngoma.
-Hii ni vifaa ambayo hutumika katika kupigia mziki.

ii) Wanyama.
-Pia hawa ni sehemu mojawapo ya makundi ya ala za mziki ambazo huweza kutoa sauti za mziki

iii) Binadamu.
-Huweza kutoa sauti linganifu ambayo hutumika kwenye kutoa sauti za mziki.

iv) Ndege.
-Pia sehemu mojawapo ya makundi ya ala za mziki huweza kutokea.

**Kielelezo Na. 4.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 4

Katika Kielelezo Na. 4.2 mtahiniwa alifafanua vitu ambavyo vinaweza kutoa sauti za muziki badala ya makundi ya ala za muziki.

### 2.1.5 Swali la 5: Sanaa za Maonesho


Swali liliwataka watahiniwa kueleza kwa ufupi faida nne za sanaa za maonesho nchini Tanzania. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 4,332 (99.49%) walipata 3.0 hadi 4.0, watahiniwa 10 (0.23%) alama 2.0 hadi 2.5 na watahiniwa 12 (0.28%) alama 0.0 hadi 1.5 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5**

| Na. | Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 1. | 0.0 – 1.5 | 12 | 0.28 |
| 2. | 2.0 – 2.5 | 10 | 0.23 |
| 3. | 3.0 – 4.0 | 4,332 | 99.49 |

Ufaulu wa jumla wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni mzuri kwa kuwa watahiniwa 4,342 (99.73%) walifaulu kwa kupata kuanzia alama 2.0 hadi 4.0.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sanaa za maonesho. Watahiniwa hao walieleza mchango wa sanaa za maonesho nchini Tanzania kama vile: *Hudumisha utamaduni, huelimisha jamii, huburudisha jamii, huhifadhi historia ya jamii* na *kurithisha maarifa, stadi na ujuzi kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine.* Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.


5

1. Chanzo cha ajira, Sanaa za maonyesha zinachangia sana katika upatikanaji wa ajira kwa hiyo vijana hujiajiri kupitia sanaa za maonyesho kama uimbaji, uigizaji majigambo, uchoraji pamoja na uchongaji

2. Huelimisha jamii, sanaa za Maonyesho huelimisha jamii kupitia Maigizo mbalimbali, michezo


3. Sanaa za maonyesho huburudisha jamii walau huburudika kupitia kuangalia Maigizo, uchoraji na mapambo mbalimbali

4. Sanaa za Maonyesho huonya jamii, sanaa za maonyesho huonya jamii kupitia ujumbe mbalimbali uliopo kwenye kazi hiyo.

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walishindwa kuchambua faida nne za sanaa za maonesho kama ilivyohitajika katika swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walichambua faida mbili za sanaa za maonesho na wengine walichanganya majibu sahihi na majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza faida za sanaa za maonesho na manufaa ambayo serikali inaweza kupata kwa kuwekeza katika sanaa za maonesho na hivyo walipata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu wengi wao walishindwa kubaini matakwa ya swali hivyo walichambua sifa za sanaa za maonesho badala ya manufaa yake. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa aliandika: *Huwasilishwa ana kwa ana katika utendaji wake, huwa na dhana inayotendeka,* na *huwa na fanani na hadhira wakati wa kuwasilishwa* ambazo ni sifa za Sanaa za maonesho kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.



5
(i) Hujenga kumbukumbu ya muda mrefu kwa wanafunzi.
(ii) Hurahisisha ufundishaji kwa mwalimu
(iii) Hutoa fursa kwa wanafunzi kujifunza kwa kutumia milango ya fahamu. mfano macho
(iv) Huchochea ari ya mwanafunzi kupenda kujifunza

**Kielelezo Na. 5.2:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5.*

Katika Kielelezo Na.5.2 mtahiniwa alieleza faida ambazo zinapatikana kutokana na kutumia mbinu shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji darasani badala ya faida za sanaa za maonesho nchini Tanzania.

### 2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Ufundishaji

Swali liliwataka watahiniwa kueleza kwa ufupi mikakati minne ya kuondoa changamoto za tofauti za usawa wa kijinsia shuleni. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 3,788 (87.00%) walipata 3.0 hadi 4.0, watahiniwa 387 (8.89%) alama 2.0 hadi 2.5 na watahiniwa 179 (4.11%) alama 0.0 hadi 1.5. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Kiwango cha ufaulu wa jumla wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 4,175 (95.89%) walifaulu kwa kupata kuanzia alama 2.0 hadi 4.0.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya usawa wa kijinsia na walielewa matakwa ya swali hivyo waliweza kueleza kwa ufupi mikakati ya kuondoa changamoto za tofauti za usawa wa kijinsia shuleni. Watahiniwa hao walieleza baadhi ya mikakati hiyo kama vile: *Kuchanganya wanafunzi wa kike na wakiume kwa idadi sawa katika vikundi vya kujifunza mfano vikundi vya majadiliano, kutouliza maswali kwa upendeleo kama vile kuelekeza maswali kwa wavulana au wasichana tu, kuchanganya wavulana na wasichana kwa idadi sawa katika michezo yoyote watakayocheza* na *mifano ya darasani isiegemee upande wa jinsi moja tu, kwa mfano mambo mabaya yasiandame wavulana au wasichana tu*. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.

6

i) kuwashirikisha wanafunzi katika michezo mbalimbali bila kuangalia jinsia.
ii) Wakati wa ukaaji wao darasani kuwapanga kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.
iii) Wakati wa ufundishaji darasani kutumia mbinu za kazi kwa vikundi kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.
iv) kuchagua viongozi ambao watakuwa katika jinsia zote mbili. jinsia za kike na zakiume hii itasaidia kuwepo kwa usawa wa kijinsia shuleni.

**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walieleza hoja pungufu ya zilizotakiwa na baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa alibaini mikakati miwili tu wakati mtahiniwa mwingine alichanganya mikakati ya kuondoa changamoto za tofauti za usawa wa kijinsia shuleni na viashiria ambavyo vinaonesha uwepo wa tofauti za usawa wa kijinsia shuleni.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya usawa wa kijinsia. vilevile, watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali hivyo kueleza majibu yasiyo sahihi. Baadhi ya watahiniwa walieleza mikakati ambayo inachochea uboreshaji wa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji shuleni. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa alitoa hoja kama vile: *Kujiunga katika kazi mbalimbali, kuwapa mazoezi na maswali, kushiriki katika midahalo* na *uanzishwaji wa michezo mashuleni*. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.

6


i) Kuwepo kwa uhuru wa kijinsia na usawa.
ii) Kuwepo na sheria.
iii) Kuwepo na adhabu.
iv) Kuwepo elimu kuhusu umuhimu wa usawa wa kijinsia.

**Kielelezo Na. 6.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 6.

Katika Kielelezo Na. 6.2 mtahiniwa alieleza ushauri wa namna ya kudhibiti usawa wa kijinsia shuleni badala ya mikakati ya kuondoa changamoto za tofauti za usawa wa kijinsia shuleni.

### 2.1.7 Swali la 7: Maandalizi ya Ufundishaji


Swali liliwataka watahiniwa kueleza kwa ufupi nyaraka nne muhimu ambazo mwalimu anapaswa kuziandaa kabla ya kuingia darasani. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 3,451 (79.26%) walipata 3.0 hadi 4.0, watahiniwa 807 (18.53%) alama 2.0 hadi 2.5 na watahiniwa 96 (2.20%) alama 0.0 hadi 1.5 kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwa kuwa watahiniwa 4,258 (97.79%) walifaulu kwa kupata alama 2.0 hadi 4.0.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maandalizi ya ufundishaji hususani nyaraka muhimu ambazo mwalimu anapaswa kuziandaa kabla ya kuingia darasani. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa na watahiniwa hao ni kama vile: *Andalio la somo, azimio la kazi, shajara ya somo, zana za kufundishia na kujifunzia* na *nukuu za somo za kufundishia.* Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.




7 - Nyaraka nne (04) muhimu anazopaswa kuziandaa ni;
(i) Azimio la kazi
- huu ni mpango kazi wa muda mrefu anaoandaa mwalimu kwa muda wa mwezi au muhula mzima.
(ii) Andalio la somo
- Ni mpango kazi wa muda mfupi anaoandaa mwalimu kabla ya kuingia darasani.
(iii) Nukuu za somo / Tini za somo
- Ni maudhui ambayo yaliyoko katika kitabu cha kiada ambayo anapaswa kuyaandaa kwa kifupi.
(iv) Zana za kufundishia na kujifunzia
- Ni vifaa au vitu vinavyopatika katika mazingira halisi.

**Kielelezo Na. 7.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 7.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu nyaraka muhimu ambazo mwalimu anapaswa kuziandaa kabla ya kuingia darasani. Watahiniwa hao walishindwa kueleza nyaraka zote nne kama zilivyohitajika katika swali. Baadhi ya watahiniwa walichanganya nyaraka sahihi na zisiszo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa *muhtasari wa somo* ni nyaraka anayoiandaa mwalimu kabla ya kuingia darasani jibu ambalo siyo sahihi. Muhtasari wa somo ni nyaraka inayoandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania kumuongoza mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walishindwa kubaini matakwa ya swali na hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya nyaraka muhimu anazopaswa kuandaa mwalimu kabla ya kuingia darasani. Baadhi yao walieleza manufaa anayopata mwalimu kwa kuandaa na kutumia nyaraka mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji badala ya kueleza nyaraka muhimu ambazo mwalimu anapaswa kuziandaa kabla ya kuingia darasani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza faida anazozipata mwalimu kwa kuandaa na kutumia andalio la somo darasani kwa hoja kama vile: *Humsaidia mwalimu kufundisha kwa mtiririko mzuri*, *humsaidia mwalimu kujiamini wakati wa kufundisha*, *humsaidia mwalimu kutotoka nje ya mada* na *humsaidia mwalimu kutumia muda wake vizuri*. Watahiniwa wengine walieleza zana za upimaji pamoja na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *Orodha hakiki, fomu ya uchunguzi, kazi mradi* na *mkoba wa kazi*. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.



7

Mambo anayopaswa kuziandaa kabla ya kuingia darasani

(i) Idadi ya wanafunzi: hakikisha mwalimu anapoingia darasani lazima ajue Idadi ya wanafunzi wake ili aweze kuandaa zana

(ii) Ukubwa wa Darasa: Darasa lenye wanafunzi wengi ni vigumu sana Mwalimu kutaka kufanyia tathmini la somo kwa usahihi

(iii) Uzingatiaji wa umri na uelewa wa Mwanafunzi katika Mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji


(iv) Ubora wa zana: Lazima zana bora ujue ni kwa kiasi gani hutumika, kujua kiwango fulani cha ufundishaji na ujifunzaji kufikiwa

**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya jibu lisilosahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7.2 mtahiniwa alieleza mambo ya msingi ambayo mwalimu anapaswa kuyazingatia kabla ya kuandaa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji darasani badala ya nyaraka muhimu ambazo mwalimu anapaswa kuziandaa kabla ya kuingia darasani.

### 2.1.8 Swali la 8: Upishi


Swali liliwataka watahiniwa kueleza kwa ufupi kanuni nne za upishi wa chakula ambazo mpishi anapaswa kuzingatia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 sawa na asilimia 100 ambapo watahiniwa 3,200 (73.50%) walipata 3.0 hadi 4.0, watahiniwa 714 (16.40%) alama 2.0 hadi 2.5 na watahiniwa 440 (10.10%) alama 0.0 hadi 1.5. Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Watahiniwa wengi 3,914 (89.90%) katika swali hili walifaulu kwa kupata alama 2.0 hadi 4.0.


Watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu upishi hususani kanuni za upishi wa chakula ambazo mpishi anapaswa kuzingatia. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali hivyo walieleza kanuni za upishi kama vile: *Kuimarisha usafi ili kuepusha maambukizi ya magonjwa*, *kubeba vifaa vyote kwa uangalifu na kuvipanga sehemu zake*, *kufunika vyakula vilivyopikwa na kuvihifadhi sehemu safi na salama kwa usalama*, *kuzima moto baada ya kupika na kama ni umeme zima swichi na mashine katika jiko ili kuepuka madhara ya moto*, *kufunika kichwa anapopika au kugawa chakula* na *kuvaa aproni safi na kukausha mikono kwa taulo safi kila siku.* Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.




**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 8.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao yaliyosababisha kutopata alama za juu. Baadhi ya mapungufu hayo ni kama; kueleza kanuni chache kinyume na matakwa ya swali, kurudia na kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi.

Vile vile, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya swali kwa kueleza majibu yasiyo sahihi. Wengine hawakuwa na maarifa kuhusu kanuni za upishi. Baadhi ya watahiniwa walieleza aina mbalimbali za mapishi ya chakula badala ya kanuni za upishi ambazo mpishi anapaswa kuzingatia. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa aliandika: *Kukaanga, kuoka, kuchemsha* na *kuchoma*. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.




**Kielelezo Na. 8.2:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 8.*

Kielelezo Na. 8.2 mtahiniwa alifafanua hatua ambazo mpishi anapaswa kuzifuata wakati wa upishi badala ya kanuni za upishi wa chakula ambazo mpishi anapaswa kuzingatia.

### 2.1.9 Swali la 9: Kilimo, Ufugaji na Uvuvi


Swali liliwataka watahiniwa kufafanua kwa ufupi faida nne za kujihusisha na shughuli za ufugaji. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 4,182 (96.05%) walipata 3.0 hadi 4.0, watahiniwa 152 (3.49%) alama 2.0 hadi 2.5 na watahiniwa 20 (0.46%) alama 0.0 hadi 1.5 kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9**

| Na. | Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 1. | 0.0 – 1.5 | 20 | 0.46 |
| 2. | 2.0 – 2.5 | 152 | 3.49 |
| 3. | 3.0 – 4.0 | 4,182 | 96.05 |

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 4,334 (99.54%) walifaulu kwa kupata kuanzia alama 2.0 hadi 4.0.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Vile vile, watahiniwa hao walibaini matakwa ya swali hivyo waliweza kufafanua kwa usahihi faida za kujihusisha na shughuli za ufugaji kama vile: *Kupata chakula kama vile nyama, maziwa na mayai; kupata pesa baada ya kuuza mazao ya mifugo na mifugo, kupata mbolea kwa ajili ya kuendeleza kilimo, chanzo cha ajira na kuongeza kipato* na *kupata malighafi kwa ajili ya kutengeneza bidhaa na mapambo kwa mfano; manyoya ya kuku hutumiia kutengeneza mapambo, ngozi za wanyama hutumika kutengeneza mikanda, ngoma na viatu.* Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.



9 (i). Kutupatia chakula mfano Nyama: Kutokana na ufugaji wa mifugo mbalimbali hutupatia chakula.

(ii): Chanzo cha mbolea ya asili: Kutokana na vinyesi vya wanyama kama vile ng'ombe nakadhalika.


(iii): Kutupatia malighafi mfano ngozi: Ambazo husaidia kutengenezea mikanda au viatu.

(iv): Chanzo cha kipato cha mtu mmoja au serikali: kutokana na fedha tunazipata kwa kuuza mifugo.

**Kielelezo Na. 9.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 9.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walishindwa kueleza kwa usahihi faida nne za kujihusisha na shughuli za ufugaji. Baadhi ya watahiniwa walifafanua faida chache na wengine walichanganya faida sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa alitoa hoja kama vile: *Ni chanzo cha kujipatia kipato (ajira), kupata kitoweo (nyama), kuwa na mifugo wengi* na *ni fahari kwa jamii.* Hoja za *chanzo cha kujipatia kipato (ajira)* na *kupata kitoweo (nyama)* ni majibu sahihi lakini hoja za *kuwa na mifugo wengi* na *fahari kwa jamii* hayakuwa majibu sahihi, hivyo alipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walishindwa kubaini matakwa ya swali hivyo kutoa majibu kinyume na walivyoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua mambo ya kuzingatia kabla ya kuanzisha shughuli ya ufugaji kama vile: *Kuwa na banda imara la mifugo, chakula kwaajili ya malisho ya mifugo, usalama wa mifugo* na *kuchanganya mifugo mbalimbali*. Watahiniwa wengine walifafanua hoja ambazo zinajirudia katika maelezo ya hoja nyingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua: *Inasaidia kupata fedha, kuweza kujimudu kimaisha, inasaidia kupata maendeleo* na *inasaidia kutokomeza umasikini uliokithiri.* Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilosahihi katika swali hili.


9


- Husaidia katika kivutio cha utalii
- Husaidia katika kuendesha shughuli mbali mbali za maisha
- Huwasaidia katika kuwakinga wanyama na maradhi mbali mbali au ndege.

**Kielelezo Na. 9.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.2 mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ufugaji hivyo alifafanua hoja zisizo sahihi.

### 2.1.10 Swali la 10: Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo


Swali liliwataka watahiniwa kuainisha vifaa vinne vya uchoraji kisha kubainisha kazi kwa kila kimoja. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 3,874 (88.98%) walipata 3.0 hadi 4.0, watahiniwa 364 (8.36%) alama 2.0 hadi 2.5 na watahiniwa 116 (2.66%) alama 0.0 hadi 1.5. Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Ufaulu wa jumla wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 4,238 (97.34%) walifaulu kwa kupata alama 2.0 hadi 4.0.

Watahiniwa waliokuwa na faulu mzuri, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Usanii wa Picha hivyo, waliweza kuanisha kwa usahihi vifaa vya uchoraji na kisha kuonesha kazi kwa kila kifaa. Vile vile, ufaulu huo mzuri ni kielelezo kuwa watahiniwa walielewa vema matakwa ya swali hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi kama ifuatavyo; *(a) Penseli - ni kifaa cha uchoraji kinachotumika kuchorea kwa mara ya kwanza, (b) Rangi - hutumika kupaka michoro picha zilizochorwa, (c) Karatasi/manila - hubeba fremu ya picha na pia juu yake picha huchorwa, (d) Raba au kifutio - hutumika kufuta sehemu zilizokosewa ili kufanya marekebisho* na *(e) Chaki - hii pia hutumika katika kuchora picha.* Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.


10 Vifaa vya uchoraji vinavyotumika katika usanii wa picha

(i) Penseli
Hii hutumika katika kuchora michoro ambayo inahitajika.

(ii) Ufuto
Hii hutumika kufuta pale ambapo pamekosewa katika uchoraji.

(iii) Karatasi au sehemu ya kuchorea.
mfano huwezi kuchora bila kuwa na sehemu ya kuchorea mchoro huo.


(iv) Rangi
Hii hutumika katika kupendezesha mchoro ambao umekwisha chorwa.

**Kielelezo Na. 10.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 10.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya usanii wa picha hivyo waliainisha vifaa pungufu ya vilivyotakiwa na baadhi yao walichanganya vifaa sahihi na visivyo sahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alianisha vifaa viwili vya uchoraji na kazi kwa kila kimoja. Watahiniwa wengine walianisha vifaa vinne vya uchoraji

lakini walishindwa kueleza kazi ya kila kifaa hivyo kushindwa kupata alama zote nne.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walishindwa kubaini matakwa ya swali na pia hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uchoraji wa picha hivyo kuainisha majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa alianisha vifaa vya uchapaji badala ya vifaa vya uchoraji kama vile: *Kimia, stensili, fremu* na *muhuri.* Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.


10
i. Apecha → kusogeza mkanda
ii. shata → kubonyeza kitufe
iii. lensi → kurekebisha mwanga
iv. Ohomu ya mbele ya uso wa kamera → kupiga picha.

**Kielelezo Na. 10.2:** Sampuli jibu lisilo sahihi katika swali la 10.


Katika Kielelezo Na. 10.2 mtahiniwa alifafanua sehemu zinazounda kamera na kazi kwa kila moja badala ya vifaa vya uchoraji na kazi zake.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha

Sehemu B ilikuwa na maswali ya insha manne (04) kutoka katika mada za: *Ushonaji wa Nguo, Upimaji, Ufundishaji wa Mada Teule* na *Biashara Ndogo ndogo*. Kila swali lilikuwa na alama 15 ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu (03) ambayo ni ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 15.0, ufaulu wa wastani alama 6.0 hadi 10.0 na ufaulu hafifu alama 0.0 hadi 5.5.

### 2.2.1 Swali la 11: Ushoni wa Nguo

Swali liliwataka watahiniwa kueleza hatua sita muhimu ambazo fundi anapaswa kuzingatia kabla ya kutarizi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 793 (18.21%) walipata 10.0 hadi 15.0, watahiniwa 2,889 (68.90%) alama 6.0 hadi 10.0 na watahiniwa 672 (12.88%) alama 0.0 hadi 5.5. Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Ufaulu wa jumla wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 3,682 (87.11%) walifaulu kwa kupata alama 6.0 hadi 15.0.


Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani baadhi walieleza hatua chache ikilinganishwa na hatua sita zilizohitajika katika swali na wengine walichanganya hoja sahihi na zisiszo sahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya utarizi wa nguo pamoja na uwezo wao katika kubaini matakwa ya swali. Watahiniwa hao walieleza kwa ufupi maana ya neno kutarizi na kubainisha aina za kutarizi katika sehemu ya utangulizi wa swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa: *kutarizi ni sanaa ya kupamba kwa kufuma mapambo kwenye kitambaa kwa kutumia nyuzi za rangi mbalimbali kwa kutumia mikono au cherehani. Kutarizi kunaweza kuwa kwa kufuma mishono ya aina mbalimbali kama vile; kikonyo, mnyororo, mjazo na mwiba wa samaki*. Katika kiini cha swali, watahiniwa walieleza hatua muhimu ambazo fundi anapaswa kuzingatia wakati wa kutarizi kama vile: *Kuandaa nguo ya kutarizi*, *kuandaa vifaa vya kutarizia*, *kuchora michoro unayotakiwa kutarizi*, *kuchagua na kukusanya nyuzi za rangi, kuchagua mshono* na *kubana nguo kwenye ringi la kubania*. Katika hitimisho la swali mtahiniwa mwingine alifafanua kwa ufupi mambo ya

kuzingatia ili kufanya utarizi mzuri kwamba, *"ili kutarizi vizuri, fundi anapaswa kuanza kutarizi nguo, foronya au kitambaa kwa mkono au cherehani wakati wa kutarizi lazima tutekeleze kanuni za ushonaji kama namna sahihi ya kushika sindano, kuwamba sindano kuelekea kwako ili usijitoboe na kuvaa subana ili kuepuka kujitunga sindano".* Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.

11

Kutarizi ni Kitendo cha Kuweka mapambo katika
nguo kwa kutumia ~~uz~~ na sindano. Mshonaji atadiona kwa
kumudio ndio sehemu anayoweka pambo hilo. Mfano wa ma-
pambo ni kama, ua, Mimba wa samaki. Zifuatazo ni
hatua ambazo fundi anapaswa kuzingatia wakati wa
kutarizi;-
Kuandaa vifaa ~~vif~~. Hii ni hatua ya mwanzo ka-
bisa ambayo fundi anapaswa kuzingatia anapofanya
utarizi. Katika hatua hii fundi ataandaa vifaa vyote am-
bavyo vinahitajika ~~W~~wakati wa kutarizi. Mfano, Uzi, sindano
cherehani.
Kuandaa nguo inayotakiwa kufanyiwa utarizi. Hatu-
a inayofuata fundi ataandaa nguo ambayo anataka kufa-
nyia ~~Utarif~~ utarizi, kama ni chafu aisafishe kwanza
kabla ya kuanza kutarizi.
Kuamua kuwa ni umbo gani ~~anat~~ atalitarizi
katika nguo hiyo. Baada ya fundi kutambua nguo ana-
yotakiwa kuitarizi ataamua kuwa ni pambo gani atali-
tarizi katika nguo hiyo. Katika hatua hii fundi atachagua
umbo lolote kutokana na nguo aliyokuwanayo.
Kuweka uzi katika sindano. Baada ya fundi
kufanya maamuzi ya umbo atakalo litarizi katika nguo-
hatua inayofuata ni kuweka uzi katika sindano amba-
po katika njia hii fundi atangiza uzi utakaotosha wa-
kati wa kufanya utarizi.
Kuanza kutarizi. Hatua inayofuata baada ya
kuweka uzi ni kuanza kutarizi kutokana na umbo alilo-
lichagua fundi kwa~~anza~~ kushona kwa kumudia mdo-
ri umbo hilo litokee kwanza mwanzo mpaka mwi-
sho, uzi utakapo isha kabla ya umbo kumalizika fundi
ataongeza uzi mwingine.


11 Cont. Kukata nyuzi zilizojitokeza juu katika umbo lililotarizwa. Baada ya fundi kumaliza kutarizi atachunguza kama patakuwa na uzi uliojitokeza katika umbo alilotarizi aukate ili usije kusababisha umbo hilo kuharibika. Hivyo basi; Baada ya kufanya hivyo atakuwa amesha kamilisha utarizi kwenye nguo itakuwa na mapambo mbalimbali yaliyotarizwa. Hivyo ili kukamilisha umbo hilo ni vyema kufuata hatua kwa hatua wakati wa kutarizi.

**Kielelezo Na. 11.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.1 mtahiniwa aliweza kueleza hatua sita muhimu ambazo fundi anapaswa kuzingatia kabla ya kutarizi.

Aidha, watahiniwa 672 waliokuwa na ufaulu hafifu walishindwa kubaini matakwa ya swali hivyo kuandika majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kiini cha swali, alieleza majibu yasiyo sahihi ambayo ni: *Kujua aina ya kitambaa au nguo anayokwenda kutarizi, maumbo au mapambo yanayotakiwa kuwekwa kwa ajili ya kuwekwa, kujua rangi atakazotumia za uzi, kujua idadi ya nguo anazotakiwa kutarizi, kuchagua mishono* na *kuwa na vifaa vyote atakavyotumia wakati wa kutarizi.* Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi.


| 11 | Kutarizi ni utraji wa nakshi katika nguo kwa kutumia uzi na sindano. Zipiotaro ni hatua sita muhimu ambazo fundi anapaswa kuzingatia wakati wa kutarizi. |
|---|---|
| | Uzi za rangi mbalimbali; fundi kabla ya kutarizi anapaswa kuwa na uzi za rangi mbalimbali kwa sababu katika kutarizi tunatumia uzi katika utraji wa nakshi hivyo fundi anapaswa kuzingatia uwepo wa uzi za rangi mbalimbali. |
| | Maumbo ya mapambo; pia fundi anapaswa kujua katika utraji huo wa nakshi ni maumbo ya rangi gani atakayo shona ili kutanya umbo livutie au nguo ivutie. |
| | Kuanza kuchora kwa kutumia uzi wenye rangi moja ili kuonesha namna umbo litakavyo kuwa; hii humsaidia atakaposhona ajue mchoro wa utraji nakshi wangu utakavyokuwa. Kwa kutumia sindano. |
| | Kutumia cherehani ya kutarizia na uzi wenye rangi mbalimbali kutarizi maumbo yako ili kuleta michoro au maumbo yanayovutia. |
| | Kutumia sibana ya mkono kukata nyuzi zote za pembeni ili maumbo yaliyoshonwa nakshi yabaki yakionekana vizuri. |
| | Kusafisha eneo la kazi; tunasafisha eneo la kazi ili libaki safi kwa ajili ya shughuli zingine kwa sababu hatuwezi kuacha sehemu ya kazi ikiwa chafu. |
| | Hivyo; ni muhimu kwa fundi wa kutarizi kutumia uzi wa rangi mbalimbali katika kutarizi ili kupanga maumbo yako yavutie. |

**Kielelezo Na. 11.3:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.2 mtahiniwa alieleza vifaa vya ushonaji na namna vinavyotumika katika utarizi badala ya hatua muhimu ambazo fundi anapaswa kuzingatia kabla ya kutarizi.

### 2.2.2 Swali la 12: Upimaji

Swali liliwataka watahiniwa kuchambua faida sita ambazo mwalimu wa somo la Stadi za Kazi anaweza kuzipata kwa kutunza kumbukumbu za matokeo ya upimaji wa wanafunzi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 3,325 (76.37%) walipata 10.0 hadi 15.0, watahiniwa 1,006 (23.10%) alama 6.0 hadi 10.0 na watahiniwa 23 (0.53%) alama 0.0 hadi 5.5 kama ilivyooneshwa katika Chati Na. 9.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12*

Ufaulu wa jumla wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 4,321 (99.47%) walifaulu kwa kupata kuanzia alama 6.0 hadi 15.0.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Upimaji hivyo waliweza kuchambua kwa usahihi faida za kutunza kumbukumbu za matokeo ya upimaji wa wanafunzi. Watahiniwa hao katika utangulizi walieleza kwa ufupi maana ya utunzaji wa kumbukumbu za matokeo ya upimaji wa wanafunzi na katika kiini cha swali, walichambua faida za kutunza kumbukumbu za matokeo ya upimaji wa wanafunzi kama vile: *Humsaidia mwalimu kutambua mafanikio na madhaifu ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji anazozitumia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi, humsaidia mwalimu kumsaidia mwanafunzi kubadili tabia za usomaji ambazo zinaathiri maendeleo yake katika mchakato wa ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi, humsaidia mwalimu kupata fursa ya kutazama kama kuna baadhi ya maudhui ya somo la Stadi za Kazi yamefundishwa ipasavyo, humsaidia mwalimu wa somo la Stadi za Kazi kuangalia ubora wa nyaraka za ufundishaji na ujifunzaji amabazo anazitumia, humsaidia mwalimu kumsaidia mwanafunzi kutambua aina ya masomo ambayo anafanya vizuri*

*zaidi na hivyo kubaini maeneo anayoweza kuongeza jitihada zaidi kukabiliana na changamoto ambazo masomo anayoshindwa kuwa na ufaulu mzuri* na *husaidia mwalimu kuwashauri wazazi na wathibiti ubora kupata taarifa za matokeo ya wanafunzi amabayo husaidia kubaini maendeleo ya kitaaluma*. Katika hitimisho, mtahiniwa alipendekeza njia ambazo mwalimu wa somo anaweza kuzitumia kutunza kumbukumbu za upimaji. Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi katika swali hili.

12


Utunzaji wa kumbukumbu za Matokeo ya upimaji wa wanafunzi, ni mchakato wa kuhifadhi taarifa mbalimbali za wanafunzi kuhusu tabia na utendaji ~~kazi~~ kazi katika taaluma mashuleni taarifa hizo zinaweza kuwa ni Matokeo ya mitihani, mahudhurio na uwajibikaji wa wanafunzi. Hoja zifuatazo zinaeleza faida anazoweza kuzipata Mwalimu kutokana na utunzaji wa kumbukumbu za matokeo ya upimaji wa Mwanafunzi.

Humsaidia Mwalimu kubaini na kufahamu Maendeleo ya wanafunzi kitaaluma, Ili Mwalimu aweze kufahamu Maendeleo ya wanafunzi wake kitaaluma anapaswa kuhifadhi na kutunza kumbukumbu za Matokeo ya upimaji wa wanafunzi wake kitaaluma

Humsaidia Mwalimu kujaza fomu za maendeleo ya upim wanafunzi kitaaluma mfano fomu hizo zinaweza kuwa ni Fomu za TSM9 ambapo fomu hizi hujazwa katika madarasa ya mitihani ya Taifa hasa zaidi katika darasa la saba.

Humsaidia Mwalimu kuandaa vyeti vya wanafunzi wanapohitimisha masomo, Kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi kitaaluma zinapohifadhiwa na Mwalimu huweza kutumika katika kutoa vyeti mbalimbali kwa watahiniwa wanapohitimisha mafunzo mfano vyeti vya Taaluma, vyeti vya nidhamu na vyeti vya uongozi bora.

Humsaidia Mwalimu katika kutoa tuzo au zawadi (motisha) kwa wanafunzi, Utunzaji wa kumbukumbu za matokeo ya wanafunzi kitaaluma hutumika katika utoaji wa tuzo na zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri kiwa ujumla.



12 Cont.

Humsaidia Mwalimu Kufahamu maendeleo ya Mwanafunzi mmoja mmoja kitaaluma katika darasa, utunzaji wa kumbukumbu kumbukumbu kumbukumbu za matokeo ya wanafunzi katika upimaji humwezesha Mwalimu kufahamu uwezo wa Mwanafunzi mmoja na Mwanafunzi Mwingine kitaaluma.

Humsaidia Mwalimu Kufanya tathimini ya somo katika ufundishaji wake, Mwalimu anapohifadhi kumbukumbu kumbukumbu za matokeo ya upimaji humwezesha kufanya Tathimini na Maboresho katika ufundishaji na uwasilishaji wa somo lake kutokana na kuona makosa mbalimbali kwa wanafunzi.


Ni vyema sana kwa Walimu wote kujitahidi kuhifadhi na kutunza kumbukumbu kumbukumbu za Maendeleo ya matokeo ya wanafunzi kupitia mchakato wa upimaji kitaaluma kwa ajili ya mafunzi ya baadaye.

**Kielelezo Na. 12.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 12.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani baadhi yao walichambua faida chache ambazo mwalimu wa somo la Stadi za Kazi anaweza kuzipata kwa kufanya upimaji wa wanafunzi ikilinganishwa na faida sita zilizohitajika katika swali. Watahiniwa wengine ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha walichanganya faida ambazo mwalimu wa somo la Stadi za Kazi anaweza kuzipata kwa kutunza kumbukumbu za matokeo ya upimaji wa wanafunzi na faida za mwalimu kufanya maandalizi ya ufundishaji.

Kwa upande mwingine watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walishindwa kubaini matakwa ya swali na wengine kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Upimaji hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipendekeza mbinu za upimaji ambazo mwalimu anaweza kuzitumia kuboresha upimaji wa wanafunzi darasani badala ya faida ambazo mwalimu wa somo la Stadi za Kazi anaweza kuzipata kwa kutunza kumbukumbu za matokeo ya upimaji wa wanafunzikama vile: K*uboresha mbinu za ufundishaji ili kuboresha changamoto ya matokeo, kuboresha zana za ufundishaji na ujifunzaji, kuwauliza maswali darasani*

*ili kutambua walioelewa na wasioelewa, mwalimu kuwatazama wanafunzi kubaini usikivu mzuri wa wanafunzi* na *mwalimu kutengeneza ukaribu na wanafunzi ili kutatua changamoto zao*. Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.


12 Mazoezi ya ufundishaji kwa muda mrefu ni ufundishaji wa muda mrefu kwa vitendo ambao mwalimu tarajali anakuwa katika eneo la kazi na kujifunza kwa vitendo kwa muda uliopangwa kwa kufanyiwa upimaji katika utendaji kazi ambayo ni kazi ya ufundishaji na ujifunzaji shuleni zifuatazo ni faida anazopata mwalimu huyo ni kama

Humsaidia mwalimu mwanafunzi katika kupata uzoefu kwa walimu wenzake au [illegible] huyo basi nafasi hizo ya walimu kwa vitendo huwapata uzoefu katika kufanya kazi ya ufundishaji kulinganisha na ufundishaji wake

Humsaidia mwalimu kupata ujuzi mpana na mbinu katika kufanya kazi ya walimu kwa upande wa [illegible] ambazo anafikiwa kuwa nazo awepo katika mazingira mbalimbali huyo ni vyema kufanya kazi ufundishaji wa vitendo

Humsaidia mwalimu kujua ufanisi wake katika kufanya na kutenda kazi yake ya ufundishaji kwa vitendo huyo basi ni vyema kufanyika kwa walimu wote tarajali


Humsaidia mwalimu kuwa na mahiri wa kufanya maandalizi ya ufundishaji mfano maazimio andalio shajara na ne pia uchambuzi wa mtaala

**Kielelezo Na. 12.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 12.

Katika Kilelezo Na. 12.2 mtahiniwa alichambua faida ambazo mwalimu tarajali anazipata kwa kufanya mazoezi ya ufundishaji wa muda mrefu badala ya faida ambazo mwalimu wa somo la Stadi za Kazi anaweza kuzipata kwa kutunza kumbukumbu za matokeo ya upimaji wa wanafunzi.

### 2.2.3 Swali la 13: Ufundishaji wa Mada Teule

Swali liliwataka watahiniwa kueleza mbinu shirikishi ambazo huwafanya wanafunzi kujifunza kwa vitendo. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 2,883 (66.21%) walipata 10.0 hadi 15.0, watahiniwa 1,365 (31.35%) alama 6.0 hadi 10.0 na watahiniwa 106 (2.43%) alama 0.0 hadi 5.5. Chati Na. 10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.





**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 13*

Ufaulu wa jumla wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 4,237 (97.56%) walifaulu kwa kupata kuanzia alama 6.0 hadi 15.0.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, waliweza kubaini matakwa ya swali hivyo waliweza kueleza kwa ufupi maana ya mbinu shirikishi na kubainisha mifano ya mbinu shirikishi katika sehemu ya utangulizi. Katika kiini cha swali walitoa hoja kama vile: *Kazi binafsi, bungua bongo, igizo dhima, majadiliano, ziara ya mafunzo, ufuatiliaji katika vikundi* na *tathmini rika.* Katika kuhitimisha swali, watahiniwa walifafanua kwa ufupi faida za

kutumia mbinu shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi. Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


13

Mbinu shirikishi ni mbinu ambazo hutumiwa na mwalimu katika kurahisisha Ufundishaji wake juu ya lengo hilo ambazo Zinawashirikisha wanafunzi katika mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji wa mada mbalimbali darasani kwahi mwalimu ili kurahisisha Ufundishaji wake anashauriwa kutumia mbinu ambazo zinawashirikisha wanafunzi katika kuchangia maarifa yao. Zifuatazo ni mbinu shirikishi zinaweza kutumiwa na mwalimu.

Majadiliano katika vikundi; Hii ni mbinu ambayo mwalimu anandaa makundi mbalimbali darasani na kuwapatia kazi ya kufanya katika makundi hayo na baada ya hapo wanafunzi kuwasilisha kile walichojadili kwenye makundi yao na mwalimu kuweza kuwakosoa walipokosea na kuwaongezea maarifa au Ujuzi zaidi.

Igizo dhima; Hii ni mbinu ambayo inawashirikisha wanafunzi kwa mwalimu huandaa igizo lipi linalohusiana na kile wanacholenga kujifunza darasani na mwalimu kufanyia baadhi ya kushiriki kwenye

13 Cont. igizo hilo hivyo kuwatanya wanafunzi kujifunza kwa vitendo zaidi juu ya kile walicho kusudia kujifunza.

Onesho mbinu; Hii pia ni mbinu ambayo ni shirikishi kwani mwalimu huweza kuwaonyesha wanafunzi mambo mbalimbali yanayotanyika katika mazingira yanayowazunguka wanafunzi mfano kumbukuzi mbalimbali zinazohusiana na na suala ambalo wamekusudia kujifunza darasani. Mfano, ma kumbusho mbalimbali yaliyo katika maeneo yao na hata kujifunza zaidi.

Bungua bongo; Hii ni mbinu ambayo inatumiwa na mwalimu darasani kwa kuuliza maswali kila mmoja na kujibu kile anacho kielewa kuhusiana na lengo wanalotaka kujifunza darasani hivyo huwatanya wanafunzi kujenga kumbukumbu za kudumu na hata kuwa wadadisi.

Mbinu ya Ziara; Hii ni mbinu ambayo mwalimu anandaa mazingira ya kufanyia ziara kuhusiana na jambo wanalotaka kujifunza mfano kuandaa eneo kwa ajili ya ziara ya kimafunzo kuhusu Utuaji kwa hivyo


13 Cont.
wanafunzi watatoka kwenye mazingira
ya shule na kwenda/ kufanya
ziara ya Ufugaji huko
kwa wafugaji.
Mbinu ya maswali na majibu;
Hii pia ni mbinu ambayo ni
mwalimu kuwauliza wanafunzi maswali
mbalimbali yanayohusiana na
somo au lengo husika analotaka
ila kulifanikisha kwa wanafunzi
hivyo hufanya wanafunzi
kushiriki katika suala zima la
Ufundishaji na Ujifunzaji na
kurahisisha Ufundishaji kwa
wanafunzi kwani wanashiriki
kuuliza na kujibu maswali hayo.
Katika Ufundishaji kwa
mwalimu anayetumia mbinu ya
mai zinazoshirikisha wanafunzi
huwafanya wanafunzi kupata
faida hizi zifuatazo kuwa
wadadisi na wabunifu, kukuza
ari ya kulipenda somo na kumpenda
mwalimu, kujenga kumbukumbu
ya muda mrefu, kukuza
Ushirikiano na mahusiano mazuri
miongoni mwa wanafunzi.

**Kielelezo Na. 13.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 13.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani waliweza kubaini matakwa ya swali lakini walishindwa kueleza mbinu sita (06) shirikishi ambazo huwafanya wanafunzi kujifunza kwa vitendo. Baadhi ya watahiniwa walieleza mbinu chache na wengine walitoa maelezo yasiyojitosheleza kutetea hoja zao, hivyo walipata ufaulu wa wastani.

Hata hivyo, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walishindwa kubaini matakwa ya swali ambapo baadhi

hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alilinganisha neno mbinu na dhana mbalimbali zinazofundishwa katika somo la Stadi za Kazi na kisha kutoa hoja kama vile: *Mbinu ya upakaji rangi, mbinu ya uchoraji, mbinu ya utarizi, mbinu ya uchongaji* na *mbinu ya ufinyanzi*. Watahiniwa wengine walieleza faida ambazo mwanafunzi anazipata akifundishwa kwa kutumia mbinu shirikishi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile: *Wanafunzi kuwa na uelewa mzuri watakapokuwa wanajifunza, kuhifadhi kumbukumbu kwani ujifunzaji wa vitendo husaidia sana kwenye kutokuweza kusahau walichofundishwa*, *itawafanya wanafunzi waweze kuandaa zana ya mada hiyo bila ya mwalimu kushughulika, wanafunzi kufurahia mada kutokana na matendo, mwalimu kuokoa muda katika ufundishaji wa mada, kukuza ufanisi wa mwalimu* na *kupata ubunifu*. Kielelezo Na. 13.3 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.



13 Mbinu shirikishi ni aina ya mbinu ambayo hutumiwa na Mwalimu ~~Kati~~ kwa kuwashirikisha wanafunzi katika kujadili mambo mbalimbalo ya somo la stadi za kazi katika suala nzima la ufundishaji na ujifunzaji. Zifuatazo ni mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji;

Mbinu shirikishi ya Muhadhara. Mfano Mkusanyiko wa wanafunzi wote katika sehemu ili kuweza kuwafikisha ujumbe kwa pamoja uliokusudiwa na Mwalimu. Pia huweza kutoa fursa kwa wanafunzi kuho

Mbinu shirikishi ya vikundi. Mfano, Mwalimu hutumia akiwa yomo darasani na kugawa katika makundi ya wanafunzi watano watano ili kuweza kufikia malengo yake aliyokusudia kwa wakati huo.

Mbinu shirikishi ya Mceto. Mfano. Mwalimu kuchukua darasa moja na kuwaunganisha katika darasa moja ili kuwezesha majadiliano yao yafikiwe kwa wakati kulingana na mawazo tofautitofauti ya wanafunzi.

Mbinu shirikishi ya Mtu mmoja mmoja. Mfano, Mwalimu na Mwanafunzi kuhojiana maswali kuhusiana namna ya kutambua nguo za harini. ~~hii~~


Mbinu shirikishi ya dharura. Mfano Mwanafunzi anaposhindwa kufanya swali na kupeleka kwa Mwalimu kwonda kuelekezwa akiwa hivyo kwa namna hiyo huweza kutumia Mbinu shirikishi ya dharura kwa mada

**Kielelezo Na. 13.3:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 13.

Katika Kielelezo Na. 13.3 mtahiniwa alieleza mbinu ambazo siyo shirikishi wala haziwezeshi wanafunzi kujifunza kwa vitendo badala ya kueleza mbinu shirikishi ambazo huwafanya wanafunzi kujifunza kwa vitendo.

### 2.2.4 Swali la 14: Biashara Ndogo ndogo

Swali liliwataka watahiniwa kuchambua kanuni sita muhimu za kuzingatia katika kuanzisha shughuli ya biashara ndogo ndogo. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,354 (100%) ambapo watahiniwa 2,564 (58.89%) walipata 10.0 hadi 15.0, watahiniwa 1,589 (36.50%) alama 6.0 hadi 10.0 na watahiniwa 201 (4.62%) alama 0.0 hadi 5.5 kama ilivyooneshwa kwenye Chati Na. 11.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14*

Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 4,153 (95.38%) walifaulu kwa kupata alama 6.0 hadi 15.0.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu biashara ndogo ndogo hususani kanuni muhimu za kuzingatia katika kuanzisha shughuli hiyo. Aidha, watahiniwa hao walibaini matakwa ya swali hivyo waliweza kuchambua kanuni hizo muhimu kwa usahihi. Katika utangulizi wa swali, watahiniwa walieleza kwa ufupi maana ya biashara ndogo ndogo na mifano ya biashara hizo. Aidha, katika kiini cha swali, watahiniwa walieleza kanuni muhimu za kuzingatia katika kuanzisha shughuli ya biashara ndogo ndogo kama vile: *Kuzingatia upatikanaji wa bidhaa au huduma unazouza au kutoa, hali nzuri ya bidhaa au huduma, kuwajali wateja, kuzingatia usafi wa sehemu unayofanyia biashara,*


*kutangaza biashara au huduma* na *kuandika kumbukumbu za mapato na matumizi.* Katika hitimisho watahiniwa walitoa hitimisho lenye maana na hivyo walipata alama zote za sehemu hiyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishauri mambo ya msingi katika kuvutia wateja na kufanya biashara iwe endelevu kama vile: i*napofanyika biashara ndogo ndogo, mfanyabiashara anapaswa kuhakikisha kuwa baada ya kuleta bidhaa au huduma anatakiwa kuzipanga vizuri katika sehemu zake ili kugundua upungufu au kiasi kilichobaki wakati wote. Pia kwa kuzingatia hayo, kitendo hiki kitawavutia wateja kubaini aina ya bidhaa alizonazo*. Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali hili.

14
Biashara ndogo ndogo ni Shughuli ya
Ununuaji na uuzaji wa bidhaa mbalimbali zina
zotumia mtaji mdogo ~~na~~ ambazo huongeza kipato.
Shughuli hizi zimegawanyika katika kundi la kutoa
huduma kwa jamii, uzalishaji, na uuzaji na ununuaji
katika maduka makubwa na kuuza kwa bei ya reja reja
Zifuatazo ni kanuni za kuzingatia katika kuanzisha
biashara ndogo ndogo.
Kuwa na chanzo cha kupata mtaji, mfan
ya biashara ndogo ndogo anapaswa kutafuta sehemu
ambayo atapata mtaji wa kuendeleza Shughuli hiyo
kwa mfano kukopa katika taasisi za fedha, mshahara
binafsi au sehemu nyingine
Aina ya bidhaa kulingana na mahitaji ya
walengwa mfano, Vyakula, Urembo au vyombo vya
kupikia, mfanya biashara anapaswa kufanya uchunguzi
ni bidhaa zipi zinapendwa zaidi katika eneo la
biashara hiyo anayopanga kufanya.
Kuwa na sehemu ya uhakika ya kupata pi
bidhaa mfano uwepo wa maduka ya jumla au
Mashamba ya bidhaa au mifugo, kanuni hii huwawe
zesha mfanya biasha kuwa na uhakika wa kuwa
na bidhaa muda wote ili asipoteze wateja
Kuwa na kitabu cha kumbukumbu ya
mapato na matumizi, kitabu hiki humsaidia mfa
nya biashara kujua taarifa nzima ya uendeshaji
wa biashara yake ili asiweze kupata hasara na
kujua matumizi aliyofanya kwa kipindi cha biashara.
Kutafuta eneo au mazingira ya kuendeshea
biashara yako mfano kuwa na (-item) ambayo atawe
ka biashara yako patakapo julikana na kuwarahi
sisha wateja kuweza kupata huduma kwa wepesi

**Kielelezo Na. 14.1:** sampuli ya jibu sahihi katika swali la 14.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walishindwa kushindwa kuchambua kanuni sita muhimu za kuzingatia katika kuanzisha shughuli ya biashara ndogo ndogo. Watahiniwa hao walichambua kanuni chache muhimu tofauti na matakwa ya swali. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa alieleza kanuni tatu tu za kuzingatia katika kuanzisha shughuli ya biashara ndogo ndogo. Mtahiniwa mwingine alichanganya kanuni za kuzingatia katika kuanzisha shughuli ya biashara ndogo ndogo na faida za kujihusiha na biashara ndogo ndogo hivyo alipata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu biashara ndogo ndogo. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa alipendekeza mbinu za kuboresha mafanikio ya wafanyabiashara ndogo ndogo kama vile: *Kuwapa hamasa wasikate tamaa katika biashara zao, serikali itoe hamasa kwa wafanyabiashara wadogo wadogo kama machinga* na *serikali iimarishe ulinzi kwa wafanyabiashara wadogo.* Kielelezo Na. 14.3 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali hili.




**Kielelezo Na. 14.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 14.

Katika Kielelezo Na. 14.2 mtahiniwa alichambua vyanzo ambavyo mfanyabiashara anaweza kupata mtaji wa kuanzisha shughuli ya biashara ndogo ndogo badala ya kanuni muhimu za kuzingatia katika kuanzisha shughuli ya biashara ndogo ndogo.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada ulionesha kuwa, jumla ya mada 13 zilitahiniwa ambapo mada za *Sanaa za Maonesho* (99.7%), *Kilimo, Ufugaji na Uvuvi* (99.5%), *Upimaji* (99.5%), *Udobi* (99.4%), *Maandalizi ya Ufundishaji* (97.8%), *Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo* (97.3%), *Misingi ya ufundishaji* (95.9%), *Biashara Ndogo ndogo* (95.4%), *Ufundishaji wa Mada Teule* (94.2%), *Upishi* (89.9%), *Ushonaji wa Nguo* (87.1%) na *Ufundi* (83.6%) zilikuwa na ufaulu mzuri. Hata hivyo, ufaulu wa wastani ulikuwa katika mada ya *Muzik*i (67.9%). Aidha, hakukuwa na mada iliyokuwa na ufaulu hafifu katika mtihani wa somo la Stadi za Kazi kama inavyooneshwa katika kiambatisho.

Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa ufaulu mzuri wa watahiniwa katika mada 12 ulitokana na umahiri wa kutosha wa watahiniwa katika mada zilizo tahiniwa pamoja na uwezo mzuri wa kubaini matakwa ya swali. Watahiniwa walikuwa na maarifa ya kujenga hoja sahihi katika kujibu maswali yaliyoulizwa. Aidha, ufaulu wa wastani katika mada moja (01) ulisababishwa na watahiniwa kueleza hoja chache ikilinganishwa na idadi ya hoja zilizohitajika, kutoa maelezo yasiyo jitosheleza na kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi katika majibu yao.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika somo la Stadi za Kazi ulikuwa mzuri kwani asilimia 99.98 ya watahiniwa walifaulu. Ufaulu wa wastani ulikuwa katika swali moja (01) tu na hakukuwa na maswali yaliyokuwa na ufaulu hafifu. Vielelezo vya majibu ya watahiniwa vinathibitisha kuwa, watahiniwa walikuwa na umahiri wa kutosha katika kujibu dhana mbalimbali zilizoulizwa na walibaini matakwa ya swali hivyo kueleza majibu sahihi.

Ufaulu wa wastani katika swali la 4 lililo tahiniwa kutoka katika mada ya *muziki,* unadhihirishwa na mapungufu mbambali katika majibu ya watahiniwa kama; kueleza hoja chache kinyume na matakwa ya swali, kutoa maelezo yasiyojitosheleza na kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuongeza kiwango cha ufaulu katika mada zilizokuwa na ufaulu mzuri na mada ya *muziki* ambayo ilikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 67.9, mapendekezo yafuatayo yanatolewa ili kuboresha ufaulu wa mada hiyo:

(i) Wakufunzi wa somo la Stadi za Kazi wapatiwe mafunzo kazini ili kuwajengea umahiri wa kufundisha wanachuo mada zenye ufaulu wa wastani na mada ambazo ufundishaji na ujifunzaji hufanyika kwa njia za vitendo kama vile; *muziki, Ushoni wa Nguo* na *Ufundi*.

(ii) Karakana za vifaa vya ufundishaji wa somo la Stadi za Kazi ziboreshwe ili ufundishaji na ujifunzaji ufanyike kwa vitendo zaidi badala ya nadharia.

(iii) Wakufunzi watumie mbinu shirikishi za ufundishaji kama; Onyesho mbinu, kazi mradi, Bungua bongo, fikiri, jozisha-shirikisha, majadiliano, kualika mtaalamu, ziara ya mafunzo, igizo dhima, matembezi ya galari na maswali na majibu ili kuwajengea uwezo wanachuo kufikiri na kutenda.

(iv) Changamoto zilizobainika na kupelekea ufaulu wa wastani kama; kukosa umahiri katika mada, kushindwa kubaini matakwa ya swali na kushindwa kujenga hoja, zitatuliwe kwa kuwafundisha wanachuo namna ya kujenga hoja, kutambua mahitaji ya swali na namna ya kujibu maswali ya insha.

(v) Wakufunzi wa vyuo vya Ualimu wafanye ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia zana za ufundishaji na ujifunzaji ili kufikia lengo la ujifunzaji na ufundishaji wenye maana.

**Kiambatisho cha Pekee**

## UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA STADI ZA KAZI

| Na. | Mada | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliopata alama 40 na zaidi | Wastani | |
| 1. | Sanaa za Maonesho | 5 | 99.7 | 99.7 | Vizuri |
| 2. | Kilimo, Ufugaji na Uvuvi | 9 | 99.5 | 99.5 | Vizuri |
| 3. | Upimaji | 12 | 99.5 | 99.5 | Vizuri |
| 4. | Udobi | 3 | 99.4 | 99.4 | Vizuri |
| 5. | Maandalizi ya Ufundishaji | 7 | 97.8 | 97.8 | Vizuri |
| 6. | Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo | 10 | 97.3 | 97.3 | Vizuri |
| 7. | Misingi ya Ufundishaji | 6 | 95.9 | 95.9 | Vizuri |
| 8. | Biashara Ndogo ndogo | 14 | 95.4 | 95.4 | Vizuri |
| 9. | Ufundishaji wa Mada Teule | 1 | 90.7 | 94.2 | Vizuri |
| | | 13 | 97.6 | | |
| 10. | Upishi | 8 | 89.9 | 89.9 | Vizuri |
| 11. | Ushonaji wa Nguo | 11 | 87.1 | 87.1 | Vizuri |
| 12. | Ufundi | 2 | 83.6 | 83.6 | Vizuri |
| 13 | Muziki | 4 | 67.9 | 67.9 | Wastani |